Lengo la kuumbwa Mwanadamu

الغاية من خلق البشر

< Swahili – السواحلية – سواحيلي >

Shaykh Muhammad ibn Saalih al-'Uthaymeen
(Allah amrehemu)
سماحة الشيخ محمد بن صالح بن عثيمين (رحمه الله)

Imetafsiriwa na: Kitengo cha Lugha ya kiswahili, katika Tovuti ya IslamHouse.com
Imepitiwa na: Yunus Kanuni Ngenda.

ترجمة : فريق القسم السواحلي بموقع إسلام هاوس
مراجعة: يونس كنون نغندا

Lengo la kuumbwa Mwanadamu

SWALI:

Sheikh: Binadamu ameumbwa kwa malengo gani?.

JAWABU: Kwajina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma Mwenye kurehemu, Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu mzima, na Rehma na Amani zimshukie Nabii Muhammad (s.a.w), pamoja na Familia yake na Maswahaba zake, Baada ya hayo.

Kwa hakika kabla ya kujibu swali hilo napenda kutoa zinduo kuhusu kanuni muhimu sana katika mambo anayo yaumba Mwenyezi Mungu Mtukufu na yale aliyo yapanga.

Na kanuni hiyo imechukuliwa kutoka katika kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Na Yeye ni Mwenye kujua, Mwenye hikima). Tahrim (2).

Na kauli yake: (Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kujua, Mwenye hikima). Ahzab (1).

Na aya nyingi tofauti na hizo zinazo onyesha na kuthibitisha hikma ya uumbaji wa Mwenyezi Mungu na yale aliyo yapanga.

Maana yake: katika mambo ya kidunia na yakisheria, kwa sababu hakuna jambo lolote analo liumba Mwenyezi Mungu Mtukufu isipokuwa ndani yake kuna hikma, sawa sawa katika kuwepo jambo hilo au katika kuliondoa, na hakuna jambo analo lipanga Mwenyezi Mungu Mtukufu isipokuwa kwa hikma vile vile, sawa sawa iwe katika ulazima au katika kuharamisha au kuhalalisha.

Lakini hikma zinazo fungamana na mambo ya kidunia au ya kisheria, yawezekana tukayajuwa na yawezekana tusiyajuwi, na yawezekana baadhi ya watu wakayajua na wengine wasiyajue, hii nikutokana na elimu na ufahamu anao wapa Allah waja wake.

Ikiwa ndivyo hivyo tunasema ya kwamba: Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu kaumba Majini na Binadamu kutokana na hikma kubwa na malengo mazuri nayo ni kumuabudu Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kama alivyo sema Mwenyezi Mungu Mtukufu:(Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi). Adhariyati: (56).

Na kauli yake: (Je! Mlidhani ya kwamba tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi kwetu hamtarudishwa). Al-Muminun: (115). Na akasema: (Ati anadhani binaadamu kuwa ataachwa bure). Al-Qiyama: (36).

Na aya nyingine tofauti na hizo zinazo julisha ya kwamba Mwenyezi Mungu anayo malengo maalum katika kuumba binadamu na majini, nako ni kufanya ibada.

Na ibada ni kudhalilika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kupenda na kutukuza kwa kufanya amri zake na kujiepusha na makatazo yake katika njia iliyo elekezwa na sheria zake, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu: (Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu). Al-Bayyina: (5).

Hii ndio hikma ya kuumbwa majini na binadamu.

Kwa maana hiyo yeyote atakae fanya jeuri na kiburi kwa Mwenyezi Mungu kwa kuacha kufanya ibada, kwa hakika atakuwa ni mwenye kupuuza hikma ambayo viumbe wameumbwa kwa sababu hiyo.

Na kitendo chake hicho kinaonyesha ya kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu kaumba viumbe kwa mchezona bila ya majukumu yoyote, na yeye japo hajatamka lakini vitendo vyake vina ashiria hivyo kutokana na jeuri yake na kupinga kwake ibada ya Mola wake.